**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tano – Tarehe 23 Disemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kazi, Majukumu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kazi, Majukumu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

148. MHESHIMIWA ALI ABDULGHULAM HUSSEIN (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

Kumekuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa ziara yake katika Mkoa wa Mjini, jimbo la Jang'ombe aliwaahidi wananchi kuwajengea skuli ya maandalizi kwa kupitia mradi wa TASAF katika shehia ya Kwaalinato eneo la skuli ya Kijangwani zamani.

(a) Je, ni hatua gani zimefikia katika utekelezaji wa ahadi hiyo.

(b) Je, wananchi wa maeneo hayo watarajie ujenzi kuanza lini.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

143. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tunaishukuru Serikali yetu kwa utunzaji wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kufanya jitihada kubwa ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki ambayo ilikua haiozi.

Je, kuna mpango gani wa kupiga marufuku matumizi ya pempas ambazo nazo ni kero na haziozi.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

172. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Baadhi ya taasisi na mamlaka za Serikali zinapuuza au kuchelewa kutekeleza hukumu za Mahakama zinazohusiana na stahiki za watumishi Serikalini na wananchi kwa jumla.

(a) Ni sababu gani hupelekea Serikali kuchelewa kulipa au kutekeleza hukumu hizo hadi kulalamikiwa katika mamlaka za juu.

(b) Je, kitendo cha kuchelewa au kupuuza kulipa, hakisababishi hasara na kuishushia hadhi Serikali.

(c) Kwa nini Mamlaka au taasisi za Serikali zinawasumbua watumishi na wananchi kwa kuwacheleweshea haki ambazo ni stahiki zao.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

202. MHESHIMIWA SHADYA MOH'D SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Wajasiriamali wa Wilaya ya Chake Chake hususan kina mama walikuwa wakifanya biashara za mbele ya hoteli ya zamani ya Chake Chake ambayo hivi sasa inajulikana kama Benki ya Baclays lakini wajasiriamali hao hivi sasa wanaondoshwa na hawana mahali maalum ya kufanyia biashara zao.

Je, ni lini Serikali itawapatia sehemu maalum wajasiriamali hao ili wasihangaike na waweze kupata riziki ya kujikimu na maisha.

224. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni Serikali yetu imefanya jambo zuri la kuwapatia wajasiriamali vitambulisho vya biashara zao ili kuwasaidia, kuwatambua na kuwapunguzia mzigo wa kulipishwa ada nyingi, jambo ambalo lilikuwa likiwapunguzia kasi ya kujitegemea na kuinua biashara zao.

Lakini kwa upande wa pili zoezi hilo limewapunguzia sana mapato Manispaa na Halmashauri za Miji ambapo mjasiriamali mmoja alikua akilipa leseni kiasi cha 360,000/= kwa mwaka na hivyo analipa 30,000/- tu kwa mwezi ambapo kwa sasa Halmashauri inakosa kiasi cha Shs 330,000/- kwa kila mjasiriamali mmoja, jambo ambalo pia litawapunguzia mapato kwa kiasi kikubwa na kupunguza uwezo wao wa kutoa huduma kwa jamii.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifidia Halmashauri hizo kwa zile ada ambazo hapo mwanzo walikua wakizipata kupitia tozo za leseni mbali mbali.

(b) Kwa kuwa baadhi ya wajasiriamali waliopatiwa vitambulisho wanamiliki vibaraza zaidi ya kimoja kwenye baadhi ya masoko, Je, wajasiriamali hao watapatiwa kitambulisho kimoja kwa biashara zote au watapatiwa kila kibaraza kitambulisho kimoja.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

174. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika dhana ya kuboresha mapato kupitia makusanyo ya kodi Serikali ya awamu ya nane ilikusudia kutumia mfumo wa Electronic Fiscal Device (EFD), ambapo iliahidi ndani ya Baraza hili tukufu kuwa mwanzoni mwa mwaka 2021 mfumo huo ungetumika Zanzibar nzima baada ya kupita muda mrefu wa majaribio.

(a) Tukiwa tunaelekea mwishoni mwa mwaka hadi sasa mfumo huo utekelezaji wake ukoje.

(b) Hali ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikoje tokea kuanza kwa majaribio hadi sasa.

175. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na taarifa kuwa Serikali imebadili mfumo wa ukusanyaji wa kodi tokea ule wa zamani wa VFDs ambao umeonekana kutokuwa na tija katika ukusanyaji.

(a) Usahihi wa taarifa hizo ukoje ili wananchi wapate fursa ya kuelewa kwa kina.

(b) Serikali haioni kuwa inapoteza fedha nyingi za walipakodi kwa kununua mifumo na vifaa visivyo na uhakika ambavyo hupelekea kubadilika badilika kila wakati kabla ya kuleta tija.

(c) Ni upi sasa mbadala wa mfumo wa awali na umefanyiwa utafiti kwa kiwango gani ili kuthibitisha ubora wake na kukwepa kuiingizia hasara Serikali.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

60. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kupunguza ukali wa maisha ndani ya nchi yetu wanawake wameunda vikundi vingi vya ushirika, vikoba hata watu wenye mahitaji maalum, vikundi vyote hivi vinahitaji msaada wa Serikali ikiwa pamoja na kupatiwa mikopo.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa makundi haya kupata mikopo hiyo hasa ukizingatia makundi yaliyopo pembezoni mwa visiwa vyetu haziwafikii habari hizi.

(b) Ni vikundi vingapi vya Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja vimepata mikopo hiyo.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

12. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Timu ya Mwenge, Jamuhuri, Chipukizi, Pindua na Mkoani Stars za kisiwani Pemba zilikuwa ni tishio hapa Zanzibar na Tanzania Bara kwa ujumla. Timu hizo ziliweza kuzitikisa timu kubwa kama vile Simba, Yanga, Malindi na Small Simba. Aidha timu hizi kwa umahiri wao ziliweza pia kutoa wachezaji mahiri wakiwemo Sotoni, Eddy Abdulla, Hamoud Seif na Khamis Mafua.

Je, ni sababu zipi za msingi na za kiufundi zilizopelekea kuteremka kwa soko la timu hizi za Pemba.

80. MHESHIMIWA JUMA ALI KHATIB (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiuza ving’amuzi kupitia Kampuni ya uunganishaji maudhui ya ZMUX ili kusaidia na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi wake wa Unguja na Pemba juu ya matukio mbali mbali yanayotokea ndani na nje ya nchi yetu. Hata hivyo, imebainika kuwa wakaazi wa Wilaya ya Mkoani, Pemba wanaotumia ving’amuzi vya ZMUX wamekuwa wakipata “channels” 29 tu wakati wenzao wa Unguja wamekuwa wakipata “channels” zaidi ya 50 wakati wote wanatumia king’amuzi hicho hicho na wamelipia bei sawa na wenzao wa Pemba,

(a) Kwa nini wananchi wa Mkoani kisiwani Pemba wanaotumia ving’amuzi vya ZMUX wamekuwa wakipata “channels” kidogo ukilinganisha na wenzao wa Unguja.

(b) Je, ni lini wananchi wa Mkoani - Pemba watafaidika kwa kuona “channels” zote zinazopatikana katika ving’amuzi vya ZMUX kama wanavyofaidika wenzao wa Unguja.

(c) Je, ni mara ngapi katika mwaka, Kampuni ya ZMUX hufanya tathimini ya ubora na ufanisi wa ving'amuzi vyake kwa wateja wake na nini matokeo ya tathimini hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

95. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Siku chache zilizopita Serikali imetangaza bei mpya ya mafuta ya petroli, dizeli na nyenginezo, jambo ambalo limewatia simanzi wananchi wetu kutokana na hali ya uchumi kwa sasa bado inasuasua kutokana na mripuko wa maradhi ya Uviko 19.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea bei za mafuta kupanda kwa kipindi kifupi tu.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha bei za mafuta zinapungua ili kuwapa wananchi tahfifu ya maisha katika kipindi hichi ambacho maisha ya wananchi wetu bado ni duni.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

25. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na kauli thabiti za mara kwa mara za Serikali kuitaka jamii kuondoa manyanyaso ya watoto katika daladala wakienda skuli na wakati mwengine wa kawaida, bado kumeshuhudiwa kuwepo kwa manyanyaso na unyanyapaaji wa hali ya juu kwa watoto katika daladala.

(a) Je, Serikali ina chombo gani rasmi kinachofuatilia na kuzuia manyanyaso na unyanyapaa wa watoto katika daladala ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba.

(b) Je, ni kesi ngapi kwa mwaka 2020/2021 zimeripotiwa na ngapi zimechukuliwa hatua dhidi ya wanyanyasaji na wanyanyapaaji.

149. MHESHIMIWA ALI ABDULGHULAM HUSSEIN (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali kwa ahadi yake ya kujenga barabara za ndani katika maeneo yetu kwani kwa sasa imekuwa ni changamoto kubwa kwa wananchi wetu.

(a) Je, Serikali imepanga kujenga barabara ngapi katika jimbo la Jang'ombe.

(b) Ni vigezo gani vinatumika kuchagua barabaraza hizo.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

89. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wananchi wa shehia ya Chimba wanaishukuru na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua ya kukubali kushirikiana nao katika ujenzi wa skuli ya Chimba kwa lengo la kuwapunguzia shida za kutafuta elimu watoto wao hasa ile changamoto ya masafa marefu.

(a) Je, ni lini Serikali itachukuwa hatua ya kuwajengea madarasa mengine ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi kwa kila darasa moja.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kuwapatia walimu wa kutosha katika masomo ya sayansi na hesabati.

(c) Je, Wizara ina mpango gani wa kuanzisha na kuendeleza maabara za sayansi na maktaba katika skuli zetu za Serikali kwa Wilaya ya Micheweni.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

33. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na juhudi za Serikali kuhimiza kilimo, ni bahati mbaya kwamba bonde la Makwararani liliopo Mjananza katika jimbo la Pandani, limechukuliwa na Serikali kwa sababu ya kilimo cha umwagiliaji ambacho hakijawanufaisha wananchi waliochukuliwa mashamba yao.

(a) Je, kwa nini Serikali imechukuwa mashamba ya wananchi bila wenyewe kunufaika na mpango huo.

(b) Je, ni utaratibu gani uliotumika kuyachukuwa mashamba hayo.

(c) Ni lini na fidia gani waitarajie wananchi waliochukuliwa mashamba yao.

207. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Sekta ya kilimo na mifugo imekuwa ikipata mafanikio makubwa siku hadi siku kwa kuwepo ongezeko la wananchi kuzalisha kwa wingi. Hata hivyo, sekta hizi kwa sasa zinaendelea kuwa na changamoto nyingi ikiwemo upungufu mkubwa wa wataalamu hasa baada ya wataalamu wachache kustaafu.

(a) Je, kwa sasa Serikali ina wataalamu wangapi wa mifugo ambao ni waajiriwa.

(b) Je, Wilaya ya Micheweni ina wafanyakazi wa mifugo, mabibi na mabwana shamba wangapi wanaohitajika kuondoa huduma duni kwa sekta hii.

(c) Je, ni lini Serikali itawaajiri wafanyakazi wengine wapya wenye fani hizo na ikifahamika kuwa Chuo Cha Kilimo Kizimbani kimetoa wahitimu wengi na bado wapo mitaani.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

90. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa kuwa Jumuiya ya ZAWIO inajishughulisha zaidi na ustawi wa jamii hasa wanawake na watoto.

(a) Je, kuna uhusiano gani baina ya Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto na Jumuiya ya ZAWIO “Organization”.

(b) Je, ni mara ngapi Wizara imekaa na Jumuiya hii kuangalia changamoto na mbinu mbadala za kupunguza udhalilishaji wa wanawake na watoto.

129. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Hivi karibuni tumekuwa tukisikia vyombo vya habari kutangaza matukio ya kupotea kwa watoto na hata watu wazima kwa mazingira ya kutatanisha.

Je, Serikali imefanya uchunguzi wowote kujua nini chanzo cha matukio hayo.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

98. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Je, ni kwa kiasi gani mikakati ya SMIDA ya kuviimarisha viwanda vidogo na vile vya kati, inaisaidia taasisi binafsi zikiwemo NGOs.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

59. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya awamu ya nane imeanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu ili kuinua wavuvi na wananchi wa Zanzibar wawe na hali nzuri ya kimaisha.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani juu ya kuwapatia wavuvi vifaa kama nyavu na mashine ili kukuza kipato chao.

(b) Je, utakubaliana na mimi kuwa kuna haja ya kuwakopesha wavuvi vifaa kama vyavu na mashine.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

156. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika ziara za Kamati za Baraza la Wawakilishi imegundulika kwamba taasisi nyingi za Serikali hazina hata hati ya kumiliki maeneo yao hali ambayo inakaribisha uvamizi wa maeneo yao.

Kwa kuwa Serikali kupitia Wizara yako ndiyo yenye wajibu wa kutoa hati hizo, Je, ni jambo gani ambalo linachelewesha utoaji wa hati hizo.

## III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kazi, Majukumu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Zanzibar,**
**23 Disemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**